

LEARNING BY EAR 2009

Economics – 1st episode

SUCCEEDING IN THE BUSINESS WORLD

**Series: “ HADITHI YA VIJANA WAWILI AMBAO
WAMEFANIKIWA KIBIASHARA KWA KUTUMIA
PESA ZAO YA MATUMIZI”**

Author: Frédéric GAKPARA

Editors: Yann Durand and Sandrine Blanchard

Translator: Anne Thomas

Kis/Translation: Eric Ponda

FIRST EPISODE: “Success begins with the desire to succeed”

Characters: John (16-year-old boy, twin.)

Jane (John’s twin sister.)

Granma (Twin’s 66-year-old grandmother.)

Farmer (24-year-old man, pushing cart.)

Ayaba (19-year-old woman, Granma's domestic help.)

Learning by Ear Soundtrack

NARRATOR:

Hujambo msikilizaji mpenzi wa makala ya Learning By Ear “Noa Bongo jenga Maisha yako” yanayotayarishwa na Deutsche Welle, wakati huu tukizungumzia masuala ya Uchumi. Katika mfululizo wa vipindi hivi tutaangazia hadithi ya vijana wawili ambao ufanisi wao wa kibiashara unatokana na ukakamavu na juhuidi za kuweka akiba sehemu ya pesa zao za matumizi. Katika mfululizo wa vipindi hivi 10 kuhusu uchumi, tutafuutilizia maisha ya vijana hawa John na Jane, mapacha wa umri wa miaka 16. Tangu wampoteze Mama mzazi, mapacha hawa wameishi maisha ya hapa na pale, wanalazimika kutenga muda wa kuishi na Baba yao na muda wa kukaa na Bibi. Ni miaka mine sasa, John na Jane wamekuwa wakimsaidia Bibi yao katika biashara yake ya kuuza nguo sokoni. Wamepata ujuzi wa kutosha katika biashara na wanaamini wanaweza kusimamia vyema biashara hiyo bila ya kuwepo Bibi yao. John anapokea pesa katika kibanda hicho ilhali Jane anawasaidia wateja. Wawili hao lakini wanamua kuanzisha biashara yao ili waweze kujitegemea. Na hapo ndipo tunapoanza kuangazia safari yao ndefu katika kipindi hiki cha utangulizi **“Ufanisi hutegemea ari ya Mtu kufanikiwa katika kila analolifanya”**

Scene 1. AT GRANMA’S STALL AT THE BIG MARKET

JOHN, JANE, HANDYMAN...

ATMO: *At the market. Sellers are chatting and transporters are trying to clear a path. The bells of a trader can be heard. Further away, cars and motorbikes are honking their horns.*

- 1. . John:** Hebu fanya hesabu Jane! tuna faranga 2,800. Mikebe miwili ya njugu ni faranga 2,400, Mkaa 150. Zinabaki faranga 250. Na mifuko ? Pia tuisahau tunataka kutayarisha njugu tamu.Kwa hiyo sukari itagharimu faranga 600!

- 2. Jane:** John, Si lazima tuanze biashara na mikebe miwili. Tunaweza kugawa mkebe moja, na kisha biashara ikiimarika, tutaongezea mkebe wa ,tatu na hata kumi. Mimi naamini tutafaulu.

- 3. John:** Ni rahisi kusema!

- 4. Jane:** Na tukiachana na njugu tamu? Kwani kila mmoja sokoni anauza njugu tamu ziwe za kukaranga au kuchemsha.Tukitaka kufanikiwa lazima tuanzishe biashara tofauti. Unakumbuka harusi ya Baba mdogo Patrick.?

5. **John:** Ndio...
6. **Jane:** Bado unakumba njugu karanga tulizokula ?
7. **John:** Ehh, zilikuwa na chumvi?
8. **Jane:** Hasa ! Na hakuna mtu anayeuzua njugu za chumvi hapa John!. Sio eti rahisi lakini pia tutaonekana kuuza njugu tofauti na halisi.
9. **John:** Ndio, ni kweli Jane! Njugu zote zinazowekwa chumvi huwa tamu, hasa ukitumia na pombe. Ngoja kidogo niangalie gharama yake.
10. **ATMO:** *sound of calculator keypad*
11. **John:** Chumvi faranga 250, Mkaa 150, jumla ni faranga 400, kwa hivyo kutoka kwa faranga 2,800 tunasalia na faranga 2,400, gharama ya mkebe miwili ya njugufaranga 1,200 na tusalie na faranga 1,200.....
12. **Jane:** Tukinunua nusu mkebe wa njugu kwa faranga 600, mifuko faranga 300 bado tunasalia faranga 300 kuwapa wateja chenji yao.

13. **John:** Ngoja kidogo...
14. **ATMO:** *calculator keys*
15. **John:** 600..., ongeza 300...,ongeza 300... ni kweli inawezekana ! (*He shouts*) Dada yangu ni mwerevu!
16. **Jane:** Sawa, sawa ! Watu wanatuangalia!
17. **John:** (*He laughs*)
Hha! Hha! Hha!
18. **Jane:** (*Suffocating a laugh.*)
Unachekesha sana wewe ! (*She turns to the customers*) Habari ,.... Dada...! Hebu angalia hili rinda ni zuri...!
19. **John:** Unafikiri bibi atatukubalia?
20. **Jane:** Kinachonifurahisha ni kwamba hutupa muda wa kupumzika. Lakini hata bila ya ruhusa yake tunahitaji kupumzika. Hatuwezi kumwendea kila wakati na kumuomba pesa, sivyo?
21. **John:** Ni kweli...

- 22. Jane:** *(To the customers)*
Mzee, tuna nguo nzuri za watoto...
Tumepunguza bei, tunauza kila kitu
hasara.,Nguo na watoto Mama! Tazama hii
sketi si bei ghali...
- 23. ATMO:** *Squeaking of a cart trying to get through.*
- 24. Farmer:** Tafadhali hebu nipisheni !
- 25. Jane:** Wewe usitugonge na kutuvunjia kibanda
chetu mzee!
- 26. Farmer:** Kila mmoja afuate shughuli zake,..!
usiniharibie kazi yangu asubuhi na mapema.
Hebu nipisheni... nipisheni!
- 27. John:** Siku moja kutatokea ajali mbaya hapa na hii
mikokoteni kutu.Mujihadhari na mikokoteni hii
iliyojaa kutu msije mkashikwa na pepopunda.
- 28.**
- NARRATOR:** Hivyo ndivyo mapacha hawa walivyofikia
uamuzi wa kuanzisha biashara yao. Badaye

alasiri hiyo wanakwenda kwa bibi yao
kumuarifu kuhusu biashara ya siku....

Scene 2. AT GRANMA'S

AYABA, JOHN, JANE AND GRANMA

- 29. ATMO:** *The bell rings. A dog barks. Ayaba can be heard coming to open the gate.*
- 30. Ayaba:** *(To the dog)*
Nyamaza Robbie!Ni nani huyo?
- 31. Jane:** Ni maafisa wa Polisi! Fungua mlango haraka!
- 32. Ayaba:** Ahh ..ni Jane!
- 33. ATMO:** *Squeaking of the iron gate opening*
- 34. Ayaba:.** Karibu, Jane.. karibu, Ala, uko na John..
Habari zenu!
- 35. John and Jane:** Asante Ayaba..!. Unaendeleaje ?
- 36. Ayaba:** Naendelea vizuri. Bibi yuko jikoni.

37. **ATMO:** *Loud noise of gate shutting. Excited dog wants to play with them.*
38. **John:** Robbie! Kimbia kimbia mbele yetu ! Njoo njoo utushike!
39. **ATMO:** ***Sound of something being deep-fried gets louder as they get closer to the kitchen.***
40. **Jane:** Shikamoo Bibi!
41. **John:** Shikamooo Bibi!
42. **Granma:** Kumbe wajukuu wangu mumefika?
43. **Jane and John:** Ndio Bibi...!
44. **Granma:** Leo nimemuacha pekee ...sikuweko....?
45. **Jane:** Lakini kila kitu kilikwenda vizuri licha ya.....
46. **Granma:** Sikuwa na wasi wasi hata kidogo...! Baba yenu anaendeleaje?
47. **Jane:** Hana neno ...!

48. **John:** Unajua Bibi....?, tumepita mtihani wetu!
- 49.
50. **Granma:** Kweli ? Niambieni ukweli!
51. **Jane:** Ndio tumepita mtihani!
52. **Granma:** Aaahhhh!!! Wajukuu zangu hebu ni wabusu!
(*She hugs them*)
Oh! Ni furaha iliyoje hii! Najua mutafauli
wajukuu wangu, hata kama watu
hawawapendi. Aaahhh!
53. **Jane:** (*Very happy*)
Bibi, utaturuhusu tupumzike siku zetu za
likizo zilizosalia ?
54. **Granma:** Mukifanya nini nyumbani pekee yenu?
55. **Jane:** Tuna mpango wa kuanzisha biashara ya
kuuza njugu ufuoni na hata kwenye mabaa.
56. **Granma:** Njugu karanga...! Si bora niwalipe mnisaidia
na biashara yangu sokoni?
57. **John:** Hapana Bibi, si kwa sababu hiyo...

- 58. Jane:** Wewe umetufunza mambo mengi na tunataka kuanzisha biashara yetu wenyewe, hasa wakati tunapokuwa likizoni. Kwani bila ya kufanya hivyo hatutakomaa Bibi...
- 59. Granma:** Ni kweli, lakini niambieni kwanini mnataka kufanya biashara hiyo ufuoni na katika mabaa?
- 60. Jane:** Tulikata kauli hiyo kwasababu tunafahamu ufuoni ni sehemu inayopendwa na watu wengi hasa wakati wa likizo. Pia barabarani na hata mabaa. Sehemu hizi huwa na watu wengi wanaopendelea kula njugu hasa wanapokunya pombe.
- 61. Granma:** Wazo zuri... Lakini ningefurahi kama mtaendelea kushirikiana na kuwa pamoja!. Sawa na muwe wanalifu..!
- 62. John:** Usijali Bibi tutakuwa waanalifu.!Tutakutana tena mwendo wa saa tisa hivi kabla ya kwenda nyumbani!
- 63. Granma:** Sawa. Hebu niwakumbushe sheria za kufaulu katika biashara!

- 64. Jane:** Moja : kuwa mchangamfu na mkarimu kwa wateja.!
- 65. John:** Pili: ubora wa bidhaa unazouza na usichoke kuusifu ubora huo..
- 66. Jane:** Tatu, kusema asante kila wakati unapopokea pesa kutoka kwa wateja wako, na pia kusema tena wakati unapowarudishia chenji .
- 67. John:** Nnne: Usiwe mbadhilifu.
- 68. Jane:** Tano: Kufanya kila liwezekanalo kujenga imani na uhusiano mwema na wateja.
- 69. Granma:** Ni kweli ! Lakini hamujaniambia mtatoa wapi pesa za kuanzisha biashara hiyo...
- 70. John:** Tayari tuna akiba ya 2,800.!
- 71. Jane:** Hizo zinatoshia kuanzisha biashara .
- 72. Granma:** Humm...Kama nimewaelewa vizuri ni kwamba tayari mmekata shauri ya kuingia katika biashara.?

73.

74. **Jane:** *(Very happy, acting like a grand lady)*
Ndio tumekata shauri Bibi. Tayari sisi ni
wana biashara mashuhuri hapa mjini!

75. **ATMO:** *Everyone bursts out laughing. The dog starts barking again...*

76. **Granma:** Chukueni hizi fedha, ni faranga 1,000
muongezee mtaji wenu....

77. **John and Jane:** *(They shout)*
Aaahhh! Bibi....!Bibi...! Bibi...!

78. **Granma:** Eh, na kabla sija saha, sasa ni lini
mtaanza biashara yenu na kuniacha peke
yangu?

79. **John:** Labda.....ehh wiki ijayo ...?

80. **Jane:** Ndio wiki ijayo....

81. **Granma:** Sawa, lakini kwa sasa tusherehekee ushindi
wenu. Ayaba, nenda ukalete glasi.
Tunaandaa sherehe ndogo hapa.

82. ATMO: *John, Jane and Ayaba laugh with joy...*

OUTRO

NARRATOR: Na hadi hapo tunafika mwisho wa makala ya leo, ikiwa ni mfululizo wa vipindi vya Learning By Ear “Noa Bongo Jenga maisha yako” mada ni masuala ya Uchumi. Kwa kuchagua biashara ambayo si wengi wanaoipendelea na pia sehemu za kufanyia biashara hiyo, John na Jane wametimiza kile watalaam wanasema “utafiti wa Kibiashara” . Pia kwa kufanya hivyo ni kujiingiza katika mchezo wa Pata Potea. Yaani kuna kupata na kukosa!

Closing soundtrack to be left running after the outro and brought up

NARRATOR: Je biashara ya John na Jane itafaulu ? Ili kujua mengi, ungana nasi kwa makala mengine ya Learning By Ear “Noa Bongo jenga maisha yako ” wakati mwengine. Na Kumbuka ukipenda kusikiliza tena kipindi hiki tembelea mtandao wetu wa DW-WORLD.DE/LBE na pia ukiwa na maoni usisite kututumia. Hadi wakati tutakapoungana nawe tena Kwaheri kwa sasa.

Music to be turned up

END